Washington State Department of Social & Health Services
Transforming lives

AGING AND LONG-TERM SUPPORT ADMINISTRATION (ALTSA)
DEVELOPMENTAL DISABILITIES ADMINISTRATION (DDA)

Kukiri Majukumu Yangu Kama Mwajiri wa Watoa huduma Wangu Binafsi

Acknowledgement of My Responsibilities As The Employer of My Individual Providers

Nachagua kuhudumiwa na Mtoa huduma Binafsi (IP) anayelipwa na Idara ya Huduma za Jamii na Afya (DSHS). Naelewa majukumu yangu kama mwajiri wa IP wangu yanahusisha:

Uchunguzi wa Usuli wa Watoa huduma Wangu Binafsi:

- Naelewa kwamba IP wangu anapaswa kukidhi vigezo vya uchunguzi wa kihistoria jimboni pamoja na uchunguzi wa alama za vidole nje ya jimbo. Naweza kumwajiri IP wangu papo hapo au kusubiri matokeo ya uchunguzi wa alama za vidole. Iwapo nitamwajiri IP wangu kabla ya kurudi kwa matokeo ya alama za vidole na ikagundulika kwamba mlezi wangu hakidhi vigezo, DSHS haitaendelea kumlipa IP huyo. Nitakuwa na uamuzi wa kuchagua IP mwingine anayekidhi vigezo:

  ☐ **Ningependa kumwajiri IP wangu kwa kipindi cha hadi siku 120 huku nikisubiri matokeo ya uchunguzi wa alama za vidole. Naelewa kwamba IP wangu anapaswa kwanza kukidhi vigezo vya uchunguzi wa kihistoria ndani ya jimbo.** Uchunguzi wa kihistoria ndani ya jimbo unahusisha; (1) kumbukumbu za makosa ya jinai kutoka Idara ya Doria ya Jimbo la Washington, (2) kumbukumbu kutoka hifadhidata (database) ya Mahakama ya Jimbo la Washington, na (3) matokeo ya chunguzi kutoka mashirika ya jimbo la Washington.

  AU

  ☐ **Ningependa kusubiri hadi uchunguzi wa alama za vidole nje ya jimbo ukamilike kabla ya kumwajiri IP wangu.** Uchunguzi wa nje ya jimbo unahusisha uchunguzi wa kumbukumbu za makosa ya jinai katika majimbo mengine.

  Jina la IP: ______________________________

Nikiwa Kama Mwajiri:

- Ninapaswa kumchunguza na kumwajiri IP anayekidhi vigezo;
- Ninapaswa kuwasiliana na msimamizi wangu (case manager) ili kuhakikisha IP husika ana mkataba halali;
- Naelewa IP wangu haruhusiwi kufanya kazi iwapo atapata taarifa kutoka DSHS kuwa anapaswa kutoendelea na kazi;
- Naelewa IP wangu haruhusiwi kufanya kazi iwapo hatakuwa tena na vigezo vya kuwa IP;
- Naelewa kwamba nitapata taarifa iwapo IP wangu haruhusiwi kufanya kazi. Iwapo nitamruhusu afanye kazi baada ya tarehe ya taarifa hiyo, mimi binafsi ndiye nitakayewajibika kumlipa IP huyo;
- Ninapaswa kuhakikisha kwamba IP wangu anaweza kufanya kazi Marekani. Ninapaswa kujaza na kutunza fomu I-9. Ninaweza kuwasiliana na Tovuti ya I-9 ya Idara ya Usalama nchini Marekani, Kitengo cha Uraia na Uhamiaji (HS-USCIS) au kupiga simu namba 1-888-464-4218 iwapo nitahitaji maelezo zaidi;
- Naelewa kwamba naweza kuwasiliana na Masijala ya Rufaa ya Huduma za Nyumbani (Home Care Referral Registry - HCCR) kwa msaada wa kumpata IP. Huduma hii inapatikana katika maeneo mengi ya jimbo hili. Naweza kuwasiliana na HCRR kwa simu namba 1-800-970-5456. Naweza kupata huduma za HCRR kwenye intaneti kupitia: http://www.hcrr.wa.gov/

Kumpangia Ratiba ya Kazi IP Wangu:

- Naelewa kwamba IP wangu **hawezi** kufanya kazi zaidi ya kikomo chake cha kazi kwa juma bila ya idhini kutoka DSHS;
- Naelewa kwamba IP wangu ana kikomo cha kazi kwa juma moja tu. IP wangu hawezi kuzidisha kikomo hiki hata kama anawahudumia watu wengine zaidi yangu;
- Napaswa kuhakikisha kwamba IP wangu hafanyi kazi zaidi ya kikomo chake cha kazi kwa juma na hazidishi saa zangu za kuhudumiwa kwa mwezi;
- Napaswa kutafuta mlezi wa ziada ili kukidhi mahitaji yangu, pale nitakampomhitaji;
- Naweza kuhitajika kuajiri walezi wa ziada ili kukidhi mahitaji yangu na kuzingatia kanuni za nyongeza ya muda rasmi wa kazi;
- Ninapaswa kuhakikisha kwamba IP wangu anaelewa huduma ya malezi yangu, anaweza kutekeleza huduma ya malezi yangu, na anaweza kufanya kazi kwenye ratiba niitakayo mimi;

- Nasimamia kazi ya IP wangu. Ingawa IP wangu ana mkataba na DSHS, DSHS haimsimamii IP wangu.

Utoaji wa Glovu:

- Napaswa kumpatia IP wangu glovu kwa ajili ya utekelezaji wa huduma binafsi zinazohusisha mikono pale zitakapohitajika:
- Naweza kupata hadi glovu 200 kwa mwezi kutoka fao langu la Apple Health (Medicaid). Naweza kupata glovu zaidi ya hizo iwapo ni muhimu kimatibabu.
- Kama ninapatiwa malezi yanayosimamiwa na huduma ya Apple Health (Medicaid), naweza kuwasiliana na huduma ya usimamizi wa afya yangu au daktari wangu ili kuagiza glovu, au kutembelea https://www.hca.wa.gov/assets/billers-and-providers/13-010.pdf
- Iwapo napatiwa huduma ya Apple Health isiyohusisha malezi yanayosimamiwa naweza:
  - Kumpigia simu msambazaji wa vifaa vya kimatibabu kutoka kwenye orodha iliyopo kwenye tovuti ya Mamlaka ya Huduma za Kiafya (Health Care Authority): https://www.hca.wa.gov/assets/billers-and-providers/ffs_providers_non_sterile_gloves.pdf au
  - Kumpigia simu daktari wangu; au
  - Kupiga simu Kituo cha Huduma za Matibabu (MSC) kwa namba 1-800-562-3022. Namba hii inapatikana nyuma ya Kadi yangu ya bluu ya Huduma za Matibabu. Kwa maelezo zaidi juu ya kupata glovu tembelea tovuti ya Mamlaka ya Huduma za Kiafya (Health Care Authority) http://www.hca.wa.gov/medicaid/dme/Pages/default.aspx.

Majukumu ya Kifedha:

- Naelewa kwamba DSHS haiwajibiki kumlipia IP wangu kodi ya zuio na kodi ya mapato isipokuwa kama IP wangu atawaomba kufanya hivyo;
- DSHS inawajibika kulipa kodi ya zuio na kodi ya Hifadhi ya Jamii na Huduma za Matibabu (FICA);
- DSHS inawajibika kulipia kodi ya zuio na kodi ya ukosefu wa ajira ya serikali kuu na serikali ya jimbo (FUTA/SUTA) isipokuwa kama IP husika ni mzazi wangu au mwanangu aliye kati ya umri wa miaka 18 na 21;
- Ninapaswa kuripoti malipo yangu ya ada ya ushiriki wa huduma ya Malezi Binafsi kwa mashirika ya kodi ya serikali ya jimbo na serikali kuu iwapo:
  - Napata huduma zangu kupitia Huduma za Nyumbani na Jumuiya (Home and Community Services) au Shirika langu la Eneo Mahalia linalotoa Huduma za Wazee (AAA), na
  - Nimemwajiri IP, na
  - Nalipa ada ya ushiriki kwa huduma za Malezi yangu Binafsi.
    - Kwa maelezo kuhusu kodi, wasiliana na Huduma ya Mapato ya Ndani (Internal Revenue Service) kwa namba 1-800-829-1040 au Idara ya Hifadhi ya Ajira ya jimbo la Washington kwa namba 1-888-836-1900.

Kuwasiliana na DSHS:

- Nitawasiliana na Msimamizi wangu (Case Manager) iwapo:
  - Nina wasiwasi juu ya huduma ya malezi yangu au kuhusu ubora wa malezi ninayopata kutoka kwa IP wangu;
  - Sipati huduma ambazo IP wangu ananitoza;
  - Sipati huduma zilizoidhinishwa kwenye huduma ya malezi yangu;
  - Nataka kubadilisha au kuongeza mlezi;
  - Nahitaji msaada wa kuajiri/kumsimamia IP wangu; au
  - Nataka kumwongezea muda wa kazi IP wangu zaidi ya kikomo chake cha saa kwa juma.

Naelewa pia kwamba nina haki ya kukata rufaa iwapo DSHS itanikatalia chaguo langu la mlezi.

SAINI YA MTEJA / MWAKILISHI WA KISHERIA	TAREHE	NAMBARI YA UTAMBULISHO WA MTEJA:
JINA LA MWAKILISHI WA MZAZI LILIOANDIKWA		